# MUONGOZO RAHISI WA RAIA KUHUSU UCHAGUZI KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA MWAKA 2014




UMEANDIKWA NA JIMMY LUHENDE

Kimetolewa na
**Shirika la Kuimarisha Demokrasia na Tawala za Vijiji**
S.L.P 1631,
Mwanza
Tanzania.
Simu: +255 754 388 882
Baruapepe:actdlg@gmail.com
Tovuti: www.adlg.org.tz

Kimeandaliwa na kuhaririwa na **Jimmy Luhende**

Katuni zimechorwa na **Marco Tibasima**

© 2014

**Kijitabu hiki kimechapishwa kwa msaada wa Konrad-Adenauer-Stiftung.**
**Hata hivyo maoni yaliyotolewa ni ya mwandishi mwenyewe.**

Actions for Democracy and Local Governance

Shirika la Kuimarisha Demokrasia na Tawala za Vijiji

Konrad Adenauer Stiftung

## Utangulizi

Mwaka 1979 Bunge lilitunga sheria namba 4 ya mwaka 1979 kuhusu uchaguzi katika mamlaka za serikali za mitaa, uchaguzi huu wa viongozi wa serikali za mitaa unaratibiwa na halmashauri za wilaya katika maeneo husika, kwa maneno mengine unaratibiwa na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Uchaguzi wa serikali za mitaa utafanyika tarehe 14 Disemba 2014. Kwa kuwa Uchaguzi ni mtiririko wa matukio, ili mwananchi ushiriki vema katika uchaguzi, unatakiwa kufanya maandalizi mapema, ikiwa ni pamoja na kutambua ni tukio gani linatakiwa kufanyika, eneo ambalo tukio hilo litafanyika na siku /muda ambapo tukio litafanyika. Usipojua vema mtiririko wa matukio, haya, ushiriki wako utakuwa mdogo na utaishia kulalamika huku na kule kwa mafanikio kidogo au bila mafanikio kabisa.

Kitini hiki kinaandaliwa ili kukuwezesha kufuatilia mtiririko wa matukio, kanuni na wahusika wakuu katika utekelezaji wa matukio haya na kanuni zake. Kitini hiki kimeandaliwa kwa kuchukua maeneo machache ya kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa ili kumuwezesha mwananchi kufahamu kwa urahisi namna ambavyo uchaguzi unafanyika, ili hatimae aweze kushiriki vema katika kuchagua au kuchaguliwa.

Kanuni ambazo zimefanyiwa mapitio ili kuandikwa kwa kitini hiki ni Kanuni nne (4) za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za 2014. Kanuni hizi zimesheheni mambo muhimu yanayotakiwa kufanyika kwenye uchaguzi wa mitaa wa mwaka huu 2014. Kanuni zinajibu maswali mengi muhimu ambayo mpiga kura au mpigiwa kura anajiuliza.




Pamoja na kanuni hizi, unashauriwa usome orodha za majina ya Kata, Mitaa, Vijiji na vitongoji halali kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka huu 2014, orodha hizi zinatambulika kama:

- Notisi ya Orodha ya Kata, Vijiji na Vitongoji katika Halmashauri za Wilaya ya mwaka 2014;
- Notisi ya Orodha ya Kata na Mitaa katika Halmashauri za Miji za mwaka 2014.

Kama mtaa au kijiji au kitongoji hakipo kwenye orodha hii maana yake hakipo kisheria na hivyo eneo hilo hakuna uchaguzi, wananchi watoe taarifa kwa wadau na kwa Tume kuhusu uchaguzi unaotaka kufanyika pahala hapo.

Kuna taarifa nyingi za upotoshaji zinazagaa kuhusu uandikishwaji, kitini hiki kitakusaidia kufahamu jinsi zoezi la uandikishwaji linavyotakiwa kuendeshwa na jinsi unavyoweza kushiriki ikiwa ni pamoja na kukupatia makisio ya tarehe za kuandikishwa na wahusika wa zoezi la uandikishwaji katika mitaa, vijiji, vitongoji.

**Moja ya malengo ya kufanya uchaguzi ni pamoja na:**

- Kuwapatia wananchi na viongozi watarajiwa fursa ya kutafakari na kujadiliana kuhusu changamoto za maisha ya watu na namna bora ya kukabiliana nazo. Hasa uchaguzi ni fursa kwa wananchi kuwaambia wagombea na ni fursa kwa wagombea kusikiliza wananchi!
- Kutoa fursa kwa wananchi nafasi ya kuchagua kiongozi na pia nafasi ya kubadilisha kiongozi. Kwa maneno mengine uchaguzi ni moja ya fursa za kuwajibisha viongozi.
- Kuwakumbusha wananchi kuwa wao ndio wenye mamlaka na kwamba viongozi ni watumishi wao.
- Kuwakumbusha wananchi na wagombea kuwa kura ni mkataba baina ya mwananchi na mgombea na kwamba mgombea akishinda nafasi ya uongozi hana budi kuwajibika kwa watu.

**Kwa nini nimuhimu ukapige kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa ?**

Ibara ya nane (8) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano waTanzania (1977) inatamka wazi kuwa hii ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii. Moja ya misingi ya Demokrasia ni “uhuru wa maoni”  “ushiriki”  na pia “kupiga kura na kupigiwa kura .” Lakini pia moja ya haki za kijamii ni afya, maji, kilimo, hifadhi ya jamii na elimu. Hivyo yapo mahusiano makubwa baina ya ushiriki katika uchaguzi huru na upatikanaji wa huduma za jamii.

Hata hivyo, kila mtu/raia anatakiwa kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, hili ni hitaji la kikatiba (tizama ibara ya 21 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977. Kipengele cha pili cha ibara hiyo kinatamka kuwa “ Kila raia anayo haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye, maisha yake au yanayolihusu Taifa. Hivyo ni wazi kuwa, haki za kijamii ni suala linalomhusu kila Mtanzania na pia uchaguzi ni suala linalomhusu kila raia hasa kwa kuwa linayo mahusiano makubwa na upatikanaji wa haki za jamii. Uchaguzi unakuhusu!

Ibara hiyo hiyo ya nane (8) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano waTanzania (1977 inaendelea kwa kutaja kuwa:

a) Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi na
b) lengo kuu la serikali litakuwa ustawi wa wananchi
c) Serikali itawajibika kwa wananchi na
d) Wananchi watashiriki katika shughuli za serikali yao kwa mujibu wa masharti ya katiba

Vipengele hivi vinne na hasa (a) na (c) vinachochea nguvu ya “kura” ya mwananchi/ raia. Vipengele hivi vinawakumbusha pia viongozi watarajiwa kuwa mwananchi ndie muajiri wake. Hivyo “uchaguzi” wa serikali za mitaa ni mchakato wa kudai haki na wajibu, ni mchakato wa kuweka mkataba baina ya mpiga kura na mpigiwa kura!

**Uhusiano wa kura yako na suala la maendeleo katika mamlaka ya serikali za mitaa**

**RASILIMALI FEDHA:** Mamlaka za serikali za mtaa hupata fedha kutoka kwenye vyanzo mbalimbali, sehemu kubwa ya fedha kutokana na malipo na ruzuku kutoka serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania . Sehemu nyingine ya mapato ya serikali za mitaa ambayo hutokana na “Mapato ya vyanzo binafsi,” ikiwa ni pamoja na kodi, mikopo na michango ya wanajamii, fedha zitokanazo na viwanda,huduma,ada ya leseni,ushuru,vibali,nk. Moja ya matatizo /changamoto au migogoro katika ngazi hii ni jinsi rasiliamali fedha inavyokusanywa na inavyotumika. Sasa unahitaji kutafakari kuhusu mtu unaetaka kumchagua kama anatosha kusimamia rasilimali hii. Migogoro mingine inahusu ruzuku za maendeleao na pembejeo za kilimo, hasa mbolea ya ruzuku.

# Maswali ya kujiuliza na kutafakari kuhusu mgombea



Ni wazi kuwa moja ya jukumu la unaemchagua ni pamoja na kutatua kero au changamoto zingine kuhusu afya, elimu, upatikanaji wa maji, migogoro ya ardhi na mipaka. Unaetaka kumchagua ni lazima awe mtu ambae unadhani anaweza kukabili changamoto hizi katika kijiji, mtaa au kitongoji chako.

**Baadhi ya maneno yaliyotumika katika kanuni za uchaguzi na tafsiri zake**

"Afisa Mtendaji wa Kata" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa shughuli za Serikali katika Kata na ni pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kata.

"Afisa Mtendaji wa Kijiji" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa shughuli za Serikali katika Kijiji na ni pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kijiji

"Chama cha siasa" maana yake ni chama cha siasa kilichopata usajili wa kudumu kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa.

"Kijiji" maana yake ni kijiji kilichomo katika eneo la Mamlaka za Wilaya na ambacho kimesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya);

"Kitongoji" maana yake ni sehemu ya Kijiji kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya);

"Mahali pa matangazo ya Uchaguzi" maana yake ni sehemu iliyotengwa maalum na Msimamizi wa Uchaguzi kwa ajili ya kutolea matangazo, taarifa za Kijiji au Kitongoji na taarifa mbalimbali zikiwa ni pamoja na taarifa za Uchaguzi .

"Mkazi" maana yake ni raia wa Tanzania ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo la Kijiji au Kitongoji na ambaye ama ana kaya au anaishi katika kaya au Taasisi iliyopo katika eneo la Kijiji au Kitongoji;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya na ni pamoja na afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi

“Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi” maana yake ni Afisa Mtendaji wa Kijiji na ni pamoja na Afisa yeyote wa umma aliyeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi wakati wa Uchaguzi kuwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi

“Msimamizi wa Uchaguzi” maana yake ni Mkurugenzi, ambamo kuna vijiji vinavyofanya Uchaguzi na ni pamoja na Afisa mwingine wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

“Orodha ya wapiga kura” maana yake ni orodha ya majina ya wapiga kura iliyoandaliwa kwa mujibu wa Kanuni.

“Raia” maana yake ni raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia;

“Siku ya uteuzi” maana yake ni siku ya kutangaza majina ya wanaostahili na wasiostahili kugombea;

“Wakati wa Uchaguzi” maana yake ni muda ambao Uchaguzi wa kawaida au Uchaguzi mdogo unatakiwa ufanyike kwa mujibu wa Kanuni na unaanzia tarehe ambayo Msimamizi wa Uchaguzi atakapotoa maelekezo ya Uchaguzi na kumalizika mara baada ya kutangaza majina ya waliochaguliwa/washindi.”

**Majina na mipaka ya Vijiji na Vitongoji**

- Kwa kuwa Msimamizi wa Uchaguzi anatakiwa kutangaza majina na mipaka ya Vijiji na vitongoji vilivyoko katika eneo la Halmashauri husika katika mahali pa matangazo ya Uchaguzi siku hamsini (50) kabla ya siku ya Uchaguzi. Unashauriwa kusoma taarifa rasmi zinazohusu mipaka ya maeneo. Mipaka iliyowekwa na Msimamizi wa uchaguzi ndio mipaka rasmi.

**Wagombea na nafasi zinazopigiwa kura**

- Halmashauri ya Kijiji ina wajumbe wasiopungua kumi na watano (15) na wasiozidi ishirini na watano (25), nafasi zinazopigiwa kura ni: Mwenyekiti wa Kijiji, Wenyeviti wa Vitongoji vilivyomo katika eneo la Kijiji, Wajumbe wengine wakiwemo wanawake ambao idadi yao haitakuwa chini ya nusu ya wajumbe wote wa Halmashauri hiyo ya Kijiji.

- Afisa Mtendaji hachaguliwi pamoja na kwamba yeye ni Katibu wa Halmashauri ya Kijiji. Nafasi hii haipigiwi kura kwani mtu huyu ni miongoni mwa watumishi wa umma.
- Mwenyekiti wa mtaa na Wajumbe wa halmasahauri ya mtaa ambao idadi yake ni sita 6.

**Kuandikisha /Orodha ya Wapiga Kura**


- Msimamizi wa Uchaguzi atateua Afisa wa Umma au mtu mwingine yoyote mwenye sifa na uadilifu ambaye ataandikisha na kuandaa orodha ya Wapiga Kura siku ishirini na moja (21) kabla ya siku ya Uchaguzi.
- Watendaji wa vijiji, Mitaa na Kata hawaruhusiwi kuandikisha wala kuandaa orodha ya wapiga kura.
- Uandikishaji wa orodha ya wapiga kura utafanyika kwenye majengo ya umma na pale ambapo hakuna jengo la umma, uandikishaji utafanyika kwenye sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa amekubaliana na Viongozi wa Vyama vya Siasa.
- Vituo vya uandikishaji wa orodha ya wapiga kura vitafunguliwa saa 1:30 asubuhi na kufungwa saa kumi (10:00) jioni.
- Vyama vya siasa vinaruhusiwa kuwepo wakati wa uandikishaji wa wapiga kura.
- Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anatakiwa kubandika orodha ya wapiga kura sehemu iliyotengwa maalum na kwa ajili ya kutolea matangazo na pia anatakiwa kutunza kumbukumbu yake.
- Mkazi yeyote wa Kitongoji au vyama vya siasa vina haki ya kukagua Orodha ya wapiga kura katika muda wa siku kumi (10) tangu kubandikwa kwa orodha ya wapiga kura ili kutoa maoni juu ya usahihi wa Orodha hiyo na anaweza kuomba orodha irekebishwe kwa kuongeza jina lake au jina la mkazi au kufuta jina lililoorodheshwa kwa vile aliyeorodheshwa hana sifa ya kupiga kura.
- Kwa mujibu wa kanuni, orodha ya wapiga kura inatakiwa ibandikwe mahali pa matangazo ya Uchaguzi

**Pingamizi dhidi ya mtu kuandikishwa**

Pingamizi linawasilishwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ambaye atalitolea uamuzi na kurekebisha orodha ya wapiga kura iliyotangazwa katika muda wa siku tano (5) kuanzia tarehe ya kuwasilishwa kwa pingamizi hilo.

Mtu yeyote au chama cha siasa ambacho hakitaridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kitawasilisha rufaa kwa Msimamizi wa Uchaguzi ambaye ataishughulikia rufaa hiyo katika muda wa siku tano (5) baada ya kupokea rufaa hiyo.  Uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu rufaa iliyowasilishwa ni uamuzi wa mwisho.

## Sifa za Mpigakura ni zipi?




**Sifa za Mgombea uenyekiti wa kijiji au ujumbe wa halmashauri ya kijiji au uenyekiti wa kitongoji**

Mkazi yeyote wa eneo la Kitongoji, mtaa anaweza kugombea uenyekiti wa mtaa, uenyekiti wa Kijiji au ujumbe wa Halmashauri au uenyekiti wa Kitongoji ikiwa:-

- Ni raia wa Tanzania;
- Ana umri wa miaka ishirini na moja (21) au zaidi;
- Ana uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza;
- Ana kipato halali cha kumwezesha kuishi;
- Ni mkazi wa kawaida wa eneo husika;
- Ni mwanachama na amedhaminiwa na chama cha siasa;
- Hajawahi kupatikana na Hatia kwa kukosa Uaminifu au kuhukumiwa adhabu ya Kifungo cha miezi sita au zaidi au adhabu ya kifo; na
- Hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.

**Siku ya Uteuzi**

- Wagombea watawasilisha fomu za uteuzi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kabla ya saa kumi kamili jioni baada ya hapo fomu hazitapokelewa ili kuruhusu kufanyika kwa uteuzi wa wagombea kutokana na fomu zilizowasilishwa.

- Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa wagombea wa nafasi za Uenyekiti, Ujumbe wa halmashauri ya Kijiji katika siku zisizopungua ishirini kabla ya tarehe ya Uchaguzi.

- Uteuzi utafanyika kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi na dakika kumi na tano jioni ya siku ya uteuzi.

- Baada ya uteuzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika majina ya wagombea wenye sifa na wasio na sifa za kugombea mahali pa matangazo ya Uchaguzi.

- Ikiwa hakuna mwombaji aliyejitokeza au kama waombaji wote waliojitokeza hawana sifa zinazostahili, utaratibu wote wa uteuzi utaanza upya.

- Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Wajumbe wengine wa Halmashauri ya Kijiji watatakiwa kujiuzulu nyadhifa zao siku **tatu** (3) kabla ya siku ya kuchukua fomu za kugombea Uongozi.

**Kutengua uteuzi**
Endapo siku ya uteuzi hakutakuwa na mgombea kutokana na kifo au sababu nyingine yeyote, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi na kupanga tarehe nyingine kwa ajili ya kufanya uteuzi mpya ndani ya siku kumi (10) tangu siku uteuzi ulipotenguliwa.

**Pingamizi la uteuzi.**

- Mgombea ambaye hakuridhika na uamuzi uliotolewa au anapinga uteuzi wa mgombea ye yote, ana haki ya kuwasilisha pingamizi na kumtaka Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kupitia upya uamuzi uliofanyika ili amteue kuwa mgombea au atengue uteuzi anaoupinga na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamteua au atatengua uteuzi uliofanyika kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa katika Kanuni za uchaguzi.

- Pingamizi litawasilishwa kwa maandishi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi katika muda wa siku mbili tangu uteuzi ulipofanyika na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atasikiliza na kutoa uamuzi katika muda usiozidi siku mbili (2) kuanzia siku ya kupokea pingamizi hilo.

- Mgombea au mwakilishi wake ambaye hataridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kukata rufaa kwenye Kamati ya Rufaa katika muda usiozidi siku nne (4) kuanzia tarehe ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi

- Kamati ya Rufaa itasikiliza na kutoa uamuzi kuhusu uteuzi wa mgombea katika muda usiozidi siku nne (4) tangu siku ya kupokea rufaa.

- Mgombea au mwakilishi wake ambaye hataridhika na uamuzi wa Kamati ya Rufaa ana haki ya kufungua kesi Mahakama ya Wilaya baada ya matokeo ya Uchaguzi kutangazwa.

**Kamati ya Rufaa**
- Kamati ya Rufaa ambayo itasikiliza malalamiko ya uteuzi wa mgombea wa Uchaguzi ni kamati ambayo ipo katika kila wilaya.
- Wajumbe wa Kamati hii wanateuliwa na Katibu Tawala wa Mkoa siku saba (7) kabla ya siku ya uteuzi wa wagombea.

**Wajumbe wa Kamati ya Rufaa**

- Katibu Tawala wa Wilaya au Afisa mwingine wa umma atakayeteuliwa atakuwa Mwenyekiti;
- Afisa yoyote kutoka Taasisi ya Umma iliyoko katika Wilaya husika.
- Afisa yeyote wa umma anayefanya kazi katika ofisi ya Katibu Tawala wa Wilaya ambaye atakuwa katibu wa kamati na hatakuwa na haki ya kupiga kura.




**Kampeni za Uchaguzi  na Masharti yake**

- Kampeni za Uchaguzi zitafanyika siku kumi na nne (14) za mwisho kabla ya siku ya Uchaguzi na zitamalizika siku moja kabla ya siku ya Uchaguzi, hivyo inatarajiwa kuwa kampeni zitaanza tarehe 01/Disemba 2014 na kumalizika tarehe 13/Desemba 2014

- Mgombea, mwakilishi wake au chama cha siasa kinaweza kuitisha na kuhutubia mikutano ya kampeni kwa kufuata ratiba waliyowasilisha na ambayo itaratibiwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.
- Kanuni zinaelekeza kuwa Msimamizi wa Uchaguzi atawasilisha ratiba ya kampeni za Uchaguzi kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ambaye atahakikisha ulinzi na usalama unakuwepo katika mikutano hiyo ya kampeni.
- Ratiba ya kampeni za Uchaguzi itakayowasilishwa na Msimamizi wa Uchaguzi ni taarifa rasmi ya mikutano ya kampeni kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi.
- Kampeni za Uchaguzi zitaanza saa mbili asubuhi na zitamalizika saa kumi na moja jioni.
- Mgombea, mwakilishi wake au chama cha siasa hakitaruhusiwa kuendesha kampeni za Uchaguzi kwa kutumia **rushwa, takrima, kashfa, lugha za matusi, ubaguzi wa kijinsia, kidini, ukabila** au wa namna yoyote ile ambao matokeo yake ni kumbagua mtu.

**Utaratibu wa kupiga kura**

- Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Wajumbe wa viti maalum wanawake, utafanyika katika vituo maalumu vya kupigia kura.

- Kutakuwa na sanduku maalum la kupigia kura lililotengenezwa kwa namna itakayomwezesha mpiga kura kutumbukiza kura yake na bila ya kuruhusu kura hiyo kutolewa ndani ya sanduku hilo.

- Kabla ya kuanza kupiga kura, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawaonesha wapiga kura sanduku la kupigia kura lililowazi na atalifunga kwa lakiri kwa namna ambayo itazuia kufunguliwa bila kukata lakiri.

- Kabla ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi hajampatia mpiga kura karatasi za kupigia kura, atajiridhisha kama jina la mpiga kura limeorodheshwa katika orodha ya wapiga kura.

- Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anaweza pia kumtaka mpiga kura aoneshe kitambulisho kitakachoonesha kuwa jina la mpiga kura huyo ndilo lililomo kwenye orodha ya wapiga kura. Katika hali hiyo mpiga kura anaweza kuonesha moja ya vitambulisho vifuatavyo:

- Kitambulisho cha mpiga kura;
- Kitambulisho cha kazi;
- Hati ya kusafiria;
- Kadi ya benki;
- Kadi ya bima ya afya;
- Kitambulisho cha shule au chuo.
- Leseni ya udereva
- Kitambulisho cha Uraia

**NI MUHIMU PIA KUTAMBUA KUWA:**

- Ikiwa mpiga kura atakuwa hana kitambulisho cha aina yoyote, lakini jina lake limo kwenye orodha ya wapiga kura iliyoandaliwa kwa mujibu wa Kanuni, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamruhusu mtu huyo kupiga kura baada ya kutambuliwa na wakazi wa eneo husika.
- Kura zitapigwa kuanzia saa mbili asubuhi mpaka saa kumi jioni.
- Kura zitakuwa za siri na zitapigwa katika majengo ya umma au sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataiteua baada ya kushauriana na wagombea, wawakilishi wao au vyama vya siasa.
- Endapo atatokea mpiga kura ambaye ana ulemavu wa macho, ulemavu wowote wa kimaumbile au hajui kusoma na kuandika, anaweza kumuomba mtu aliyemchagua yeye mwenyewe kumsaidia kupiga kura isipokuwa Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Mgombea au Mwakilishi wake.
- Kura hazitapigwa katika majengo ya vyombo vya usalama na Vyama vya Siasa

**Karatasi za kura**

Karatasi za kupigia kura zitakuwa na:

- Jina la Mgombea;
- Jina la Chama;
- Nembo ya Chama; na
- Nembo ya Halmashauri husika .

**Kuhesabu kura**

Wakati wa kuhesabu kura watu wafuatao wataruhusiwa kuwepo katika kituo cha kuhesabia kura:-

- Msimamizi wa Uchaguzi;
- Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
- Mgombea;
- Mwakilishi wa Mgombea;
- Askari au Afisa wa Polisi, Mgambo wenye sare au Afisa yeyote anayesimamia ulinzi;na
- Mwangalizi wa Uchaguzi.

**MUHIMU:** Kabla ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi hajaanza kuhesabu kura atafanya yafuatayo mbele ya wagombea au wawakilishi wao:

- Atahakiki idadi ya wakazi waliopiga kura;
- Atahesabu idadi ya karatasi za kupigia kura ambazo hazikutumika na kuziweka katika bahasha maalum;
- Atakagua lakiri na kuona kama imefunguliwa au haijafunguliwa;
- Atakata lakiri; na
- Atafungua sanduku la kupigia kura.

**MUHIMU:** Kura zitahesabiwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kwenye eneo ambalo Uchaguzi umefanyika mbele ya wagombea au Wawakilishi wao.

# Utaratibu wa kutangaza matokeo




**Utaratibu wa kutangaza matokeo ya wajumbe wa Halmashauri wa kundi la wagombea mchanganyiko yaani wanawake na wanaume na wajumbe wa Halmashauri wa kundi la wagombea wa viti maalum wanawake**

- Endapo idadi ya wagombea ni ndogo kuliko nafasi za ujumbe zilizopo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza kuwa wajumbe na utaratibu wa kujaza nafasi zilizobaki utaanza;
- Endapo idadi ya wagombea ni sawa na nafasi za ujumbe zilizopo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea wote kuwa wajumbe wa Halmashauri

- Endapo idadi ya wagombea ni kubwa kuliko idadi ya nafasi za ujumbe zilizopo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea waliopata kura nyingi kuwa wajumbe wa Halmashauri na
- Endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea au kwa baadhi yao, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha kutangaza matokeo na atapanga tarehe nyingine ya Uchaguzi ili kumpata mshindi au washindi baina yao, ambao watatangazwa kuwa wajumbe wa Halmashauri
- Matokeo ya Uchaguzi wa Wajumbe wa Viti Maalum Wanawake yatajazwa kwenye fomu maalum ambayo itasainiwa na Wagombea au Wawakilishi wao pamoja na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi na kubandikwa kwenye sehemu ya matangazo na nakala kuwasilishwa Ofisi ya Serikali ya Kijiji **kwa ajili ya kujumlishwa na kutangaza mshindi au washindi .**

**MUHIMU:** Kutokuwepo kwa wagombea au wawakilishi wa mgombea wakati wa kupiga kura, kuhesabu kura, kutangaza matokeo au kukataa kusaini fomu ya matokeo hakutazuia wala kubatilisha utekelezaji wa shughuli yoyote ya Uchaguzi.

### Kuahirisha Upigaji Kura

Endapo siku ya kupiga kura litatokea tukio litakalozuia upigaji kura kuendelea kufanyika, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha upigaji kura hadi siku inayofuata au siku nyingine anayoona inafaa ili mradi zisizidi siku saba (7) tangu siku ya Uchaguzi ulipoahirishwa, **kwa maana hiyo, katika uchaguzi huu wa tarehe 14 Disemba, siku za kuahirishwa hazitazidi tarehe 21 Disemba 2014**

### Malalamiko Kuhusu Uendeshaji wa Uchaguzi

Mgombea yeyote ambaye hakuridhika na uendeshaji wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kupeleka malalamiko yake Mahakama ya Wilaya ndani ya siku thelathini (30) baada ya siku ya kutangaza matokeo ya Uchaguzi. Malalamiko haya ni yale tu yanayohusu ukiukwaji wa utaratibu wa Uchaguzi (Kanuni za uchaguzi).


Nafasi za uongozi wa serikali za mitaa itakuwa wazi endapo litatokea moja kati ya mambo yafuatayo:-
Kifo cha Mwenyekiti au Mjumbe;
Mwenyekiti au Mjumbe kujiuzulu wadhifa wake;
Mwenyekiti au mjumbe kuondokewa na sifa za kuwa mgombea;
Kubatilishwa kwa matokeo ya Uchaguzi;
Endapo mwenyekiti au mjumbe hatahudhuria mikutano mitatu ya kawaida mfululizo bila kuwa na sababu ya msingi.
Endapo mwenyekiti au mjumbe atahama Kijiji au Kitongoji;
Endapo Mwenyekiti au mjumbe atakoma kuwa mwanachama wa chama cha siasa kilicho mdhamini;
Endapo Mwenyekiti hataitisha mikutano mitatu ya kawaida mfululizo bila kuwa na sababu za msingi;
Endapo Kijiji au Kitongoji kitagawanywa.

Endapo litatokea jambo lolote kati ya hayo, ni jukumu la Afisa Mtendaji kutoa taarifa kwa Mkurugenzi katika kipindi kisichozidi siku kumi na nne (14) tangu kutokea kwa jambo hilo. Nae Mkurugenzi atatangaza kuwepo kwa nafasi wazi ya uongozi katika eneo hilo ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kupokea taarifa toka kwa Afisa Mtendaji.

- Nafasi wazi itajazwa kwa kufanya Uchaguzi mdogo kwa utaratibu uliopo katika Kanuni na itajazwa katika muda wa siku sitini (60) baada ya kutangazwa kuwa wazi.
- Hakuna nafasi itakayojazwa endapo muda uliobaki ni miezi sita (6) au pungufu yake kufikia siku ya kufanyika kwa Uchaguzi wa kawaida.

**Kiapo**

Watakao kula kiapo cha uaminifu na kutunza siri mbele ya Wakili, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao ni pamoja na Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Mwenyekiti na wajumbe wa Kamati ya Rufaa; na Afisa mwingine yeyote wa umma atakayeteuliwa kusimamia shughuli za Uchaguzi.

Viongozi wote (wenyeviti,Wajumbe wa Halmashauri ) watakula kiapo cha utii na uadilifu katika mkutano wa mtaa/ Kijiji/Kitongoji mbele ya Wakili, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya baada ya kuchaguliwa, na kabla ya kuanza kutekeleza majukumu ya uongozi.

**Watazamaji wa Uchaguzi**

Watazamaji wa ndani na wa nje watakaopenda kutazama Uchaguzi wanatakiwa kuwa na kibali cha Msimamizi wa Uchaguzi. Pia, shughuli hii ya kutizama chaguzi ina maadili na kanuni zake.

Kama ulivyosoma katika kipengele cha kuhesabu kura, watu hawa ni moja ya wateule wanaoruhusiwa kuwepo katika eneo la kuhesabu kura. Mtu yeyote anaweza kuwa mtazamaji wa uchaguzi ilimradi ana kibali kutoka kwa msimamizi wa uchaguzi.

# Yafuatayo ni makosa ya uchaguzi



1) Kuharibu orodha ya wapiga kura;
2) Kutoa taarifa za uongo ili aweze kupiga kura au kugombea uenyekiti au ujumbe wa Halmashauri
3) Kuharibu karatasi za wagombea;
4) Kughushi karatasi za uteuzi;
5) Kupiga kura zaidi ya moja kwa ajili ya kumchagua mgombea mmoja;
6) Kutishia wapiga kura au wagombea ili kuvuruga Uchaguzi;
7) Kufanya kampeni siku ya Uchaguzi;
8) Kuonesha ishara au kuvaa mavazi yanayoashiria kumtambulisha mgombea au chama cha siasa ndani ya mita mia tatu kutoka kwenye Kituo cha Uchaguzi;
9) Kumzuia Msimamizi wa Uchaguzi kutekeleza majukumu yake;
10) Kukiuka masharti ya kiapo chake;
11) Kupatikana na karatasi za kupigia kura zaidi ya moja kwa mgombea mmoja
12) Kuvunja masharti ya kampeni za Uchaguzi: na
13) Kufanya jambo lolote kinyume na Kanuni za Uchaguzi huu.

**Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Wajumbe wa** Kamati ya Rufaa au Afisa yeyote wa umma aliyehusika na usimamizi wa Uchaguzi akibainika kukiuka masharti ya kanuni na akipatikana na hatia atahukumiwa. Adhabu zake ni kifungo na faini ambazo zimeainishwa katika kanuni.

**Masuala 11 muhimu kuhusu Uchaguzi huu**

1) Tarehe ya kufanyika kwa Uchaguzi ni tarehe 14 Disemba 2014
2) Tambua muda na sehemu ya kuandikishia wapiga kura
3) Muda wa kufanya uchaguzi mahali pa kufanyia Uchaguzi katika eneo lako
4) Hamasisha wakazi wote wenye sifa za kupiga kura washiriki Uchaguzi huu muhimu
5) Hamasisha wakazi wenye umri wa miaka Ishirini na moja (21) au zaidi wanaweza kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji,ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji
6) Tarehe na muda wa kuchukua na kurudisha fomu za maombi ya kugombea uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji.
7) Muda wa kuchukua na kurudisha fomu za kugombea hautazidi siku saba (7)
8) Siku ambayo uteuzi utafanyika na mahali pa matangazo ya Uchaguzi ambapo fomu za wagombea zitabandikwa ili wapiga kura wazione.
9) Muda wa kutoa pingamizi dhidi ya uteuzi na kusikilizwa kwa pingamizi.
10) Muda wa kusikiliza rufaa dhidi ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi
11) Kipindi cha kuendesha mikutano ya kampeni za Uchaguzi, kwa mujibu wa kanunu ni siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya uteuzi (siku ambayo majina ya wanaostahili na wasiostahili kugombea yalitagazwa)

# Sifa za kiongozi ni zipi?



**Moja ya changamoto katika chaguzi**

Masula yanayotajwa sana katika chaguzi ambayo yanaweza kuathiri uchaguzi ni pamoja na:

- Wananchi kutohudhuria mikutano ya hadhara
- Wananchi kuwa na hofu ya kutokea Vurugu
- Baadhi ya wagombea au timu za kampeni kutoa rushwa, na mwananchi kukubali kupokea rushwa ile ili kupindisha haki yake ya kupiga kura na hivyo kuchagua mtu asie na sifa za kuongoza
- Watu waliojiandikisha kutojitokeza kupiga kura siku ya uchaguzi
- Kutokuwa na utaratibu mzuri wa kuwasaidia walemavu, wazee, wajawazito wakati wa zoezi la kupiga kura
- Wananchi kutolinda kura zao baada ya kupiga kura
- Kucheleweshwa kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi
- Wananchi kutokujua pahala vituo vya kupigia kura vilipo au vituo kuwa mbali sana na makazi ya watu

Kama unayo maoni yoyote kuhusu kijitabu hiki, tafadhali tuma kwa:


**Shirika la Kuimarisha Demokrasia na Tawala Vijiji na Kata**

Mkurugenzi Mtendaji
Shirika la Kuimarisha Demokrasia na Tawala Vijiji
+255 754 388 882
actdlg@gmail.com
S.L.P 1631,
Mwanza, Tanzania